# Usawiri wa Wahusika wa Jinsia ya Kiume katika Riwaya ya *Chozi la Heri*

*Miriam Bageni Mwita*[1] na *Fred John Mutwiri*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Mashariki mwa Afrika, Baraton*
[2]*Chuo Kikuu cha Chuka*

**Ikisiri**

**Fasihi ni kioo cha jamii kitumiacho lugha kwa usanii kwa kuashiria hali ya maisha katika jamii na kubainisha jinsi jamii inavyoshughulikia masuala mbalimbali. Makala haya inashughulikia usawiri wa wahusika wa jinsia ya kiume katika riwaya ya Chozi la Heri na Assumpta Matei. Lengo kuu la makala haya ni kuchunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya na aidha, kubainisha mielekeo ya wanajamii kuwahusu wahusika wa kiume. Makala haya yalijikita katika madhumuni ya kueleza matatizo yanayowakumba wanajinsia ya kiume katika riwaya ya Chozi la Heri. Nadharia ya Uhalisia imeongoza mjadala huu. Nadharia hii, iliasisiwa na tapo la wanamaendeleo. Baadhi ya waasisi wa nadharia ya Uhalisia ni kama vile; Balzac, Stendhal na Flaubert. Nadharia ya Uhalisia hutumiwa na watunzi kumulika tajriba anuwai katika jamii. Matokeo ya makala haya yalionyesha kuwa wahusika wa jinsia ya kiume wanapitia matatizo kama vile; kubaguliwa, upweke, kuharibiwa kwa mali zao, kupokonywa ardhi, kuhujumiwa, kuingizwa katika ulanguzi wa dawa za kulevya, kuibiwa, kusalitiwa, kuchochewa na kutoajiriwa. Inatarajiwa kuwa matokeo ya makala haya yatawafaa wasomi, wanajamii, na waandishi kung'amua kuwa nyakati za kumtwaza mwanaume zimeisha kwani anakumbwa na matatizo sawa na apitiayo mwanamke.**

**Maneno Muhimu:** Fasihi, Uhalisia, Uhakiki, Jinsia, Wahusika.

## Utangulizi

Kipindi cha miaka michache iliyotangulia msimu wa ulimwengu wa ukapitalisti, baraza za wanaume, majarida na makala mbalimbali ya magazeti kuhusu uume yalitolewa maradufu ili kushughulikia masuala ya jinsia ya kiume. Kujikita katika tafiti kuhusu wanawake pekee kumekashifiwa na wataalamu mbalimbali waliobainisha kuwa, kuzungumzia nafasi ya mwanamke tu kana kwamba ni wanawake tu waishio duniani, ni Upotoshi mkubwa.

Kwa mujibu wa Wandera (2002) na King'ei (2002) tafiti nyingi juu ya masuala ya uana zimezingatia nafasi ya mwanamke. Makala haya yanajadili nafasi ya mwanamume hasa kwa kuangalia anavyosawiriwa katika riwaya ya Chozi la Heri. Aidha, Flood (1990) anasema kuwa, upinzani pia umetolewa dhidi ya kushughulikia

masuala yanayohusu wanaume kwani baadhi ya watu wanaona kuwa kuyazingatia mambo hayo kutaendeleza na kudumisha dhana zilizopo za kijinsia ambapo inachukuliwa kuwa wanaume wote hufaidi kutokana na masuala ya jinsia. Tunaishi katika jamii iliyojikita kwenye mfumo wa kuumeni, mfumo ambao unaelekea kuwafaidi au kuwapendelea wanaume. Makala haya yanashikilia kuwa ni muhimu kuwashughulikia wanaume katika tafiti za kifasihi kwani ndiyo njia pekee ya kuwaelewa vyema na pia kuonyesha jinsi wanadhulumiwa katika jamii ambayo inaamini kuwa kuwa kiumbe huyu ndiye huwadhulumu wengine.

Kulingana na Morell (2005) wafeministi wengi wanahofia kujiingiza kwenye masuala ya wanaume kwani jambo hili linanuia kurudisha nyuma juhudi za wanawake. Wanasema kuna mabadiliko kadhaa yametokea ambapo baadhi ya wanaume wameanza kujizatiti kuishi kwa amani na wanawake, watoto na wao wenyewe japo wanaume wengine wameshindwa kujitambua na kutekeleza hili. Makala haya yalinuia kubainisha namna jinsia ya kiume inasawiriwa katika jamii ya Waafrika kupitia kwa riwaya ya Chozi la Heri.

**Nafasi ya Jinsia ya Kiume katika Jamii**

Kama anavyosema Gagiano (2000), waandishi wengi wa riwaya aghalabu huwa ni wachanganuzi wa jamii wanazosawiri na huwa wa kimsingi katika kuwaza na kuchunguza masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hapa, tumechunguza matatizo yanayokumba jinsia ya kiume na umuhimu wa uwakilishi wa haki za kijinsia zote. Crous (2005) anaonyesha jinsi wanawasilisha vipengele vya uume huko Afrika Kusini na vile wanachunguza mahusiano ya mamlaka kati ya wahusika wanaume na pia wa kike, kwa kuyarejelea maoni ya wanaume kuhusu jinsia. Mawazo haya yalitufaa katika kuchunguza usawiri wa mwanamume katika jamii kwa kurejelea riwaya ya Chozi la Heri, riwaya ambayo inadhihirisha udhalalishwaji wa mhusika wa jinsia ya kiume.

Libby (2012) anashughulikia suala la mfumo wa kuumeni uliojikita kwenye dini ya kikristo. Mfumo huu unasisitiza utaratibu wa utawala msonge au kingazi katika familia. Ukristo unazingatia utaratibu huu kuwa umetoka au kuamuliwa na Mwenyezi Mungu. Wanawake na wanaume wana majukumu mbalimbali ya kutekeleza ambapo mume ndiye mwenye kukimu na kulinda familia; naye mke ndiye hutarajiwa kuwalea Watoto, kando na kushughulikia majukuu ya nyumbani, kama vile upishi. Kulingana na mfumo huu, wanawake wanafaa kuwa chini ya utawala wa wanaume siku zote. Mabinti wanafaa kuwatii baba zao na wake wanafaa kuwatii waume wao. Kila mmojawao akitekeleza jukumu lake alilopewa na Mungu basi familia itastawi. Basi, mfumo wa kuumeni wa kikristo ni ile imani kuwa Mungu ameamuru na kuweka utaratibu mahususi katika familia ambao unafaa kufuatwa. Mfumo huu una vipengele viwili muhimu. Kwanza, imani katika uongozi au utawala wa kiume na kisha imani kuwa wanaume na wanawake wana majukumu tofauti kabisa ya kutekeleza. Mfumo huu unashikilia kuwa mwanamke hafai kamwe endapo atashindwa kuwa chini ya uongozi wa kiume.

Walby (1990) anasema kuwa mfumo wa kuumeni ni utaratibu wa kijamii unaolenga kumtawala, kumtumia ovyo, kumnyanyasa mwanamke na kumthibiti. Viwango vya uthibiti huu hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine kwa sababu ya tofauti za kitabaka, kidini, kikabila na kitamaduni. Asasi ya dini ndiyo huupa nguvu mfumo wa kuumeni kwani inathamini utawala wa mwanamume zaidi katika jamii. Pia sheria kuhusu familia, talaka, ndoa na urithi zinahusishwa na mfumo wa kuumeni. Ni katika mkabala huu ambapo tunaangazia namna mwanamke ametwazwa katika jamii na kuchukua nafasi iliyokuwa ya mwanamume.

Chaterji (2004) anachunguza mabadiliko katika mfumo wa kuumeni akizingatia jamii ya Wahindi kule Uhindi. Anadhihirisha kuwa majukumu ya wanawake katika jamii hiyo yamebadilika kimfululizo katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Jambo hili halikufikiriwa sana hapo awali. Pia anatoa mifano ya mabadiliko ya majukumu ya wanawake na wanaume. Anaeleza kisa cha wanawake watano waliodaiwa kumwua jambazi sugu. Vile vile, mtu aitwae Yadau alichomwa kisu na kupigwa kwa mawe na kundi la wanawake. Aidha, Chatereji anaonyesha athari ya mabadiliko ya kiuana hasa katika mahusiano kama ndoa yaliyosababishwa na maendeleo ya wanawake katika masuala ya kijamii, kiuchumi, kimawazo na kisiasa duniani kote. Wanaume wanaona vigumu kuishi na wanawake wa sampuli hiyo.

Amadiume (1987), mwanasosholojia kutoka Nigeria, alishiriki kwenye utafiti katika kijiji chake cha Nobi kilichoko Kusini Mashariki mwa nchi hiyo. Utafiti wake unahusu uana na jinsia katika jamii ya Kiafrika. Anatoa hoja kuwa, katika jamii ya kabla ya ukoloni, jinsia na uana hazikugongana. Anachunguza miundo ambayo iliwawezesha wanawake kupata nguvu na akaonyesha kuwa majukumu hayakusemekana kuwa ya kike au kiume. Utafiti wake wa jamii ya Igbo nchini Nigeria uligawanywa katika vipindi vitatu: kipindi kabla ya ukoloni ambapo mifumo ya jadi ilitenda kazi, kipindi cha ukoloni ambapo Waingereza walitawala nchi ya Nigeria na kipindi cha baada ya ukoloni wakati nchi hiyo ilipata uhuru. Anasema kuwa wanawake wangeweza kutekeleza majukumu ambayo, kwa kawaida, husemmwa kuwa ni ya wanaume. Hivyo basi, wanawake wakaitwa ‘wanaume’. Hili liliwezeshwa na hoja kuwa wanawake hawa walijitegemea kiuchumi na pia kulikuwepo na dini iliyowaangazia wanawake. Gitau (2005) anachunguza suala la unyanyasaji dhidi ya wanaume katika riwaya mbili na tamthilia mbili. Aliangazia mwandishi mmoja wa kike na watatu wa kiume. Mtafiti huyo anaonyesha misingi na aina za unyanyasaji dhidi ya wanaume. Aina hizi ni Pamoja na kudhulumiwa kimapenzi na kupigwa.

**Matokeo ya Utafiti**

Makala haya yalipangwa kwa kuzingatia lengo la mahsusi: Matatizo yanayowakumba wahusika wa jinsia ya kiume. Matokeo hayo yaliwasilishwa kwa kutumia majedwali. Maelezo pia yalitolewa ili kuweka wazi matokeo kuhusiana na matatizo yote yaliyochunguzwa.

**Matatizo yanayowasibu wahusika wa jinsia ya kiume**

Usawiri ni jinsi wahusika wa jinsia ya kiume wanaumbwa na kuendelezwa katika riwaya husika ili kuwakilisha nafasi ya jinsia ya kiume katika fasihi. Wahusika wa jinsia ya kiume wamesawiriwa kwa njia mbalimbali.

**i) Hukumu ya kifo dhidi ya mwanamume, hata mume ambaye atapatikana na kosa la kumbaka mke wake**

Tunaarifiwa kuwa Kaizari anaanza kusimulia yaliyojiri siku ile baada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya kana kwamba Ridhaa alikuwa mgeni wa hayo. Anasema kuwa baada ya kutawazwa kwa kiongozi mwanamke, mambo yaliharibika. Watu wakashika silaha kupigania uhuru wao, uhuru ambao walidai hawakupewa wakaupigania. Mwanaharakati Tetei alitoa kauli kuwa, wanaume watatumikishwa kama walivyofanywa enzi za kiistiimari katika visakale vya majirani wao walipokuwa wakiongozwa na mwanamke wa kiimla. Anasema kuwa wanawake walikuwa wakiwatumikisha wanaume kutifua udongo mashambani huku wanawake wameketi kama majeta. Tetei anaonekana kukerwa na jinsi haki za jinsia ya kike zinavyotiliwa maanani bila kujali jinsia ya kiume kama vile; *Affirmative action* na *a third should be Women*. Aidha katika kila kikao anasema utasikia kidudumtu akisema;

> *…fikiria suala la jinsia. Na usidhani ni jinsia nyingine, ni dada zetu tu. Vikao vya kupigania haki vinapigania elimu ya motto wa kike , haja ya kuwainua akina mama kiuchumi, hukumu ya kifo kupitishwa dhidi ya mwanamume, hata mume ambaye atapatikana na kosa la kumbaka mke wake… Uk 17*

Tetei analalamikia jinsi ambavyo jinsia ya kike imepewa mamlaka na jamii na kuishia kumdhalilisha mwanamume. Mwandishi alianzia kukashifu wanaharakati na vikundi mbalimbali ambavyo vimejitwika jukumu la kushughulikia jinsia ya kike huku wakisahau jinsia ya kiume. Makala haya yamebainisha kuwa, kasumba ya utaasubi wa kiume iliyokuwa enzi za kale imepitwa na wakati. Kwa sasa, kunahitaji vikundi na wanaharakati mbalimbali kwani matatizo aliyokuwa akiyapitia mwanamke ndiyo yanapitiwa na mwanamume karne hii ya ishirini na moja. Kwa hivyo, kuna hitaji la dharura kushughulikia jinsia ya kiume kwani tusipoziba ufa tutajenga ukuta. Uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na mkubwa. Mtazamo huu unatia mkazo kwenye uwasilishi wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii. Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004), nadharia ya Uhalisia huwakilisha uhalisi wa mambo katika fasihi.

**ii) Kubaguliwa kwa misingi ya kiukoo**

Kulingana na Hegel (1998) katika kitabu chake kinachojulikana kama ujumi. Mtaalamu huyu alipendekeza matumizi ya neno uhalisia kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inauwasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii ambako kuna wahusika au mhusika anayetenda mambo kwa jinsi inayochochewa waziwazi na mazingira yake.

Katika riwaya ya Chozi la Heri mhusika Ridhaa anabaguliwa kwa kuwa ametoka ukoo tofauti na watu wa ukoo wa Msitu wa Heri. Ridhaa alikuwa amesimama kwa maumivu kwa yaliyompata. Amelitazama wingu la moshi ambalo lililojikokota kwa kedi na mbwembwe, aidha, linamkumbusha ukiwa aliozaliwa nao na ambao anahofia kuwa angeishi na kuzikwa nao. Alipogeuka alitazamana ana kwa ana na tanuri la moto ambalo liliteketeza jumba lake la kifahari. Katika mkasa huu wafuatao waliangamia Terry mkewe Ridhaa, bintiye Tila, Lily Mkewe Mwangeka na mjukuu wake Becky, Ridhaa.

Aidha, tunaarifiwa kuwa hakuwa mkaazi asilia wa Msitu wa Heri. Alikuwa wa mfuata mvua kama walivyoitwa walowezi na wenyeji kindakindaki walionunua na kuhamia sehemu tofauti. Babake alikuwa na wake kumi na wawili. Wake hawa walijaliwa na wana wa kiume ishirini na ndipo ardhi ya mzee Mwimo Msubili ikawa haitoshi kuwalea madume hawa. Jambo hili limfanya mzee mwimo kuwahamishia wake wawili wa mwisho Msitu via Heri . Siku hizo ilikuwa rahisi mtu kuwa na shamba mahali kokote katika eneo lililomilikivia na kabila lake kwani umiliki wa mashamba ulitegemea bidii ya mtu.

Mamake Ridhaa alikuwa mke wa mwisho wa Mzee Mwimo. Ridhaa alikuwa mwenye umri wa miaka kumi walipohamia Mlima via Heri na alikuwa bado hajaanza shule. Walipowasili humu hamkuwa na wakaazi wengi na ilimchukua muda kuzoeana na watoto wa majirani ambao waliwaona Ridhaa na nduguze kama waliokuja kuuvuruga utulivu wao. Ridhaa alikuwa kati ya waathiriwa wa hali hii kwani alitengwa na wenzake siku ya kwanza shuleni katika michezo mbalimbali. Alichokozwa na mwanafunzi mmoja anamwambia:

> *…wewe ni Mfuata Mvua hatutaki kucheza nawe. Umekuja hapa kutushinda katika mitihani yote. Wewe ndiwe unatuibia kalamu…uk10*

Mwanafunzi aliyemwita 'mfuata mvua' na kumwambia hakutaka kucheza naye kwani alikuja kuwashinda katika mitihani yote mtunzi alidhamiria kuonyesha watoto hujifunza kwa wazazi wao kwahivyo, watoto hawa wamejifunza kutoka kwa wazazi wao kutoshirikiana na watu ambao si wajamii zao. Makala haya iligundua kuwa wanajamii wana chuki na watu mbalimbali ambao wamehamia sehemu zao hasa kwa njia ya kununua ile ardhi. Watu hawa huonekana kama maadui kwa wanajamii asilia. Ridhaa ameyafanya mengi mazuri kikijini hadi kikaacha kuitwa Kalahari. Ikawaje aliowatendea hisani wamelipa kwa madhila? lweje watu waliokula na kunywa pamoja ndio waliomlipulia aila na kuyasambaratisha maisha yake? Haya maswali yasiyo na majibu yalimsumbua akilini mwake. Alipowaza alianza kuelewa sababu ya vikaratasi kuenezwa kila mahali vikiwatahadharisha kuwa mna gharika baada ya kutawazwa kwa Musumbi- kiongozi mpya. Anaelewa sababu ya jirani kuacha kumtembelea kwake kwa ghafla. Anaelewa sababu ya mke wa jirani kulalamika kuhusu kuuzwa kwa mashamba ya wenyeji kwa wageni. Alielewa kuwa alikuwa mgeni wala si mwenyeji hata baada ya kuishi pale miongo mitano. Hatua waliyoichukua watoto hawa na familia ya mzee Kedi inawakilisha Nchi za Kiafrika kwani kuna migogoro mingi juu ya masuala ya ardhi.

**iii) Kuingizwa katika matumizi na uuzaji wa dawa za kulevya**

Dick anakumbuka siku alipoanza kusafiri kwa ndege. Siku hiyo alijawa na kiwewe kwani biashara haramu ya kubeba dawa za kulevya aliyokuwa amejiingiza kwayo ilikuwa imewaingiza wengi kwenye mikono ya polisi, wakatiwa mbaroni. Siku hizo alikuwa mwanagenzi katika uga huu kwani alikuwa na umri wa miaka kumi tu. Zipo siku alipotetemeka karibu ajisaliti lakini hatimaye alizoea kujipa moyo. Sasa miaka kumi ya adha imepita. Haukuhitaji mnyonge. Dick alitoswa katika kinamasi cha kuuza dawa za kulevya na Sauna- kijakazi wao.Dick amesafirisha maelfu kwa maelfu ya vifurushivya dawa hizi. Mwanzoni akawa si mraibu wa dawa hizi lakini ilibidi ajizoeshe kwa usalama wake mwenyewe, kwani mara nyingi alilazimika kuzimeza dawa zenyewe ili kwenda kuzitapika kwenye masoko ya ughaibuni.

Jambo hili lilichangiwa na uwepo wa mashine zenye uwezo mkubwa wa kung'amua shehena za dawa zilizofichwa kwenye chupi. Siku ile baada ya kijakazi Sauna kumwiba Dick baba mmoja tajiri ambaye alijitia kumpeleka shuleni.Kumbe alikuwa amempeleka katika biashara yakuuza dawa za kulevya. Buda (lakabu ya tajiri wakeDick) alipoona Dick akitaka kukataa kushiriki biashara hii, alimtishia Dick kuwa angetupwa nje, asingiziwewizi na bila shaka Dick alijua malipo ya wezi ni kutiwa tairi na kuchomwa moto. Wazo la kupata adhabu ya aina hii lilimtetemesha Dick. Akambuka rafiki yake Lemi alivyofishwa kwa njia hii. Kisa cha Lemi kilimfanya kuunasihi moyo wake kuingilia biashara hii haramu ili mwenye nguvu asije akamtumbukiza akajisemea kuwa huenda siku moja akapata mbinu ya kujinasua. Mwandishi anapoandika kitabu hiki, alikuwa akitaka kukashifu vitendo vya matajiri na walezi wa watoto wanaowadhulumu watoto wa jinsia ya kiume kwa kuwaingiza katika ulanguzi wa dawa za kulevya. Mhimili wa sanaa kuchukuliwa kama kioo cha kumulikia maisha halisi ya binadamu katika mazingira yake ilitumika kudadisi kama wahusika wa jinsia ya kiume yale wanayoyapitia katika riwaya ya Chozi la Heri ni yale yanayofanyika katika jamii halisi.

**iv) Kupokonywa ardhi**

Ridhaa anaelezea wimbo wake Shamsi. Anasema kuwa leo Shamsi anasikika kama amebadilisha wimbo wake kama anavyosema Ridhaa japo kwa sauti ya chini. Wimbo huu wa leo unasikika kama wa kiumbe mwenye maumivu zaidi na mapigo yake hasa ni ya mbolezi. Shamsi anaomboleza kwa kifo cha babake ambaye amekufa kwa ukosefu wa dawa hospitalini na ukosefu wa chakula jambo linalosababisha kula mizizi mwitu. Shamsi ana majonzi kwani kupitia wimbo wake tunaona kuwa bwana Mabavu alikuja na hati miliki bandia na kunyakua ardhi yao. Wanajamii wote walikimya kusiwe na yeyote wa kusema lolote. Babake alijitwika jukumu la kumsomesha huku akidhani ndiye atakayekuwa mshumaa kwa aila yake ila hapati kazi baada ya kuhitimu. Ridhaa anapomsikiliza anaksema kuwa wimbo huu wa leo ni tofauti na majigambo yake ya kila siku. Ridhaa alianza kuyaghani majigambo yake Shamsi kwa sauti ya chini kama anayeyatia maneno ya majigambo kwenye mizani.Ridhaa anamtazama Shamsi akipita kama afanyavyo kila siku.Mtaa

anakoishi Shamsi si mbali na hapa, Shamsi na Ridhaa ni majirani. Huu ni mwezi wa tatu tangu Ridhaa kuhamia mtaa wa Ahueni. Ahueni ni mtaa wa raia wenye kima cha juu kiuchumi. Mtaa huu una sura ya mijengo ya kifahari ya ghorofa.

Daraja kubwa limeutenga mtaa huu na mtaa wa Kazikeni inakoishi familia ya Shamsi na nyingine za aina yake. Huku maisha ni ya kubahatisha. Huu ni mtaa wa mabanda yaliyojengwa kwa udongo na mabati. Mwandishi anapoandika Riwaya hii ya Chozi la Heri anadhamiria kuonyesha tamaa ya walivyonavyo na jinsi wahusika wa jinsia ya kiume wanavyotesa dhidi ya dhuluma za kunyakuliwa ardhi. Maisha ya Shamsi yanabadilika na kuwa mlevi kwani anaona suluhu ya matatizo anayoyapitia yanaweza kuondolewa tu kwa kunywa pombe. Makala haya imebaini Shamsi na wahusika wengine katika Mtaa wa Kazikeni ni mfano tu wa mitaa mingi ya mabanda katika sehemu mbalimbali Barani Afrika. Mwandishi alisukumwa kuwa na nia ya kuusawiri uhalisia katika ukamilifu wake katika wakati alipoandika. Mwandishi amepenya chini ya picha za kijuujuu na kuidhihirisha mifanyiko ya mabadiliko iliyoko. Suala la uhalisia uonyesha uhusiano uliopo kati ya lugha na sura ya matendo.

**v) Kuonekana kama kiumbe kisicho na hisia**

Jinsia ya kiume pia inasawiriwa kama viumbe wasio na hisia. Ridhaa anatatizika sana na milio ya kereng'ende na bundi usiku wa kuamkia siku hii ya kiyama. Milio hii ilimtia kiwewe aidha alijaribu kumjuza mkewe ila alipuuza kwa kumwambia kuwa yeye ndiye ameishi kumwambia kuwa asishikamane na mambo ya ushirikina:

> *…anamkumbusha Ridhaa kuwa aliwahi kumwambia kuwa ni vizuri kuiacha mielekeo ya kijadi ambayo huyafifilisha maendeleo. Anazidi kumuuliza hata iwapo jambo likawa atafanya nini? Uk 17*

Ndipo Terry anamjuvya kuwa la muhimu ni kumlaani shetani kwani Iiandikwalo ndilo. Mazungumzo haya baina ya Terry na mmewe Ridhaa yalikuwa ya mwisho kabisa kutokea Terry akiwa hai. Ridhaa anatamani kuwa alikuwa na muda zaidi wa kumuuliza mkewe maswali ambayo sasa yameivamia akili yake. Machozi yalifurika machoni mwake kwa yale yaliyompata. Katika kumbukizi zake anakumbuka maneno ya marehemu mamake kuwa machozi ya mwanamme hayapaswi kuonekana mbele ya majabali ya maisha. Ila Ridhaa aliacha machozi yamcharaze yatakavyo hakujali la mama wala la baba; alijisikia kama mpigana masumbwi aliyebwagwa na kufululiziwa makonde bila mwombezi. Mamake Ridhaa anamweleza mwanawe kuwa, kulia hakuumbiwa majimbi ila makoo. Mwandishi anaonyesha mitazamo potovu waliyo nayo watu kuhusu jinsia ya kiume. Iwapo makoo wanaruhusiwa kulia basi ata majimbi wana hisia wapaswa kulia kuondoa uchungu na masikitiko.

**vi) Kuachwa katika hali ya upweke**

Lunga alipohamia Mlima wa Simba mke wake Naomi naye hakuwekwa na mazingira haya mapya. Asubuhi moja alimtumia Lunga ujumbe na kumtaarifu kuwa ameondoka ili akatambe na ulimwengu na huenda akaambulia Cha kumsaidia Lunga kuikimu familia. Akawaacha Lunga na wanawe. Pigo hili la tatu lilimuuma Iunga sana kwani alijisabilia kwa hali na mali kumpendeza mkewe. Naomi alilipa penzi lake na kumwachia Lunga adha za malezi jambo ambalo Lunga hakustahimili. Mwaka mmoja wa kwanza ulimwia Lunga mgumu mno kwani ilimlazimu Lunga kuwa mama na baba wa watoto wake. Katika hali hii Iunga aliingiwa na wahaka na kihoro na hatimaye ugonjwa wa shinikizo Ia damu ukampata. Kabla ya mwisho wa mwaka huo Lunga alifariki na kuwaacha watoto wake mikononi mwa kijakazi wao. Mwandishi anaonyesha jinsi wahusika wa kiume ambao wako katika mahusiano au ndoa wanayowapata mara tu wanapokosa hela. Lunga alikuwa tajiri wa kutajika kwani alikuwa mkurugenzi katika kampuni ya nafaka na maghala. Alipoachishwa kazi aliendeleza kilimo katika Msitu wa Mamba ila wanapofurushwa na serikali na kuenda Mlima wa Simba mkewe Naomi anaonyesha ukatili dhidi ya mmewe kwa kumuachia watoto katika hali hiyo ya kusikitisha. Makala haya imebaini kuwa Naomi ni kiwakilishi wa wanawake katika jamii ambavyo nia yao katika ndoa ni kula mali ya mumewe.

Wana wa Kangata walipokwenda shuleni walijisajilisha kwa jina Ia tajiri wa baba yao. Walikuwa wakiitwa Lunga Kiriri, Lucia Kiriri na Akelo Kiriri. Kiriri likiwa jina Ia Mwajiri wa Kangata. Kangata na mwajiri wake walikuwa wamekulia kutoka mtaa wa Matunda katika zile patashika za baada ya kutawazwa. Kiriri aliiaga dunia muda mfupi kutokana na kihoro cha kufilisika na ukiwa aliokuwa ameachiwa na mkewe Annette na wanawe. Walipata Green Card na kuhamia ughaibuni. Hivyo basi, juhucii za Kiriri kumshawishi mkewe asimnyime ushirika wa Wanawe ziliaangukia moyo wa Firauni. Mkewe Kiriri alikuwa ashaamua kuwa hapa hapamweki tena. Kazi aliyokuwa akiifanya katika afisi za umma kama mhazili mwandamizi kwa miaka mingi ilikuwa inamfanya kusinyaa, akawa hana hamu akahisi kinyaa. Wanawe walipoenda kusomea Ng'ambo wafanyavyo wana wa viongozi kwa kuwa wanaiona elimu ya humu kama isiyowahakikishia mustakabali mwema raia wake, yeye alistaafu mapema na kuchukua kibunda cha mkupuo mmoja almaarufu Golden Handshake akachukua Green Card na kuwafuata na kumwacha mume wake akiwa mpweke. Baada ya wana wa Kiriri kumaliza masomo yao walibakia huko huko Uzunguni kufanya kazi. Walipuuza rai ya baba mtu za kurudi nyumbani ili kuziendesha baadhi ya biashara zake. Kila mmoja akajishughulisha na mambo yake. Kifungua mimba wa Kiriri kwa jina Songoa alisema kuwa nchi yao haina chochote kumfaa kwa hata walio na shahada tatu bado wanalipwa mshahara mdogo sana, akaona heri awekeze huko mbali aliko na imani nako.

**Marejeleo**

Amadiume, I. (1987). *Male Daughters, Female Husbands: Gender and Sex in an African Society*. London: Zed Publishers Ltd.

Assumpta k. (2017). *Chozi la Heri*. Nairobi: One Planet Publishers.

Chaterji, S. A. (2004). Signs of Change in Patriarchal Ideas about Men and Women's Status and Role in Indian Society. Katika Gender and Conflict Transformation.Irenees.net

Crous, M. L. (2005). Presentation of Masculinity in a Selection of Male-Authored Post Apartheid Novels, University of Stellenbosch.

Flood, M. (1990). "Men Plural." www.xyonline.net/Menplural/Connell.shtml (Accessed on 13th October 2016).

Gagiano, A. (2002). *Achebe, Head, Marechera: On Power and Change in Africa*. Boulder: Lynne Rienner.

Gitau, E. N. (2005). Unyanyasaji Dhidi ya Wanaume Katika Fasihi Andishi ya Kiswahili. Tasnifu ya M.A. chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Hegels, G. W. F. (1998). *Aesthetics*. Oxford: Oxford University Press.

King'ei, G.K. (2002). "Swala la Uana Katika Fasihi ya Kiswahili: Uhakiki wa Utafiti Kutoka Kenya." Katika Utafiti wa Kiswahili. Eldoret: Moi University Press.

Libby, A. (2012). *Love, Joy, and Feminism: What is Christian Patriarchy?* An Introduction. Patheos.

Morrell, R. (2005). *Foreword to Men Behaving Differently*.In: Reid, Graeme and Liz *Walker (eds) South African Men Since 1994*. CapeTown: Double Storey.

Ntarangwi, M. (2004). Uhakiki wa Kazi za Fasihi. Rock Island Augustana College.

Walby, S. (1990). *Theorising* Patriarchy. London: Basil Black Well.

Wandera, S. (2002). "Utafiti wa maswala ya Kijinsia Katika Kiswahili." Katika Utafiti wa Kiswahili. Eldoret: Moi University Press.